

UNIUMBIE MOYO SAFI

Mtunzi : Charles NYENZE
Maneno : Zaburi 50



10



1. Unumbie moyo safi, ee Mungu,
utengeneze tena ndani yangu roho imara.
Usinitupe mbali na uso wako,
wala usiniondoshee roho yako takatifu.

2. Unirudishie furaha ya wokovu wako,
unisabitishie roho karimu.
Nitawafundisha waasi njia zako,
nao wakosefu watakuongokea.

3. Kwa maana haupendezwi na sadaka,
ningetoa sadaka ya kuteketezwa, hungeipokea;
Sadaka yangu, ee Mungu, ni roho ya kutubu:
moyo uliotubu na kupondeka, ee Mungu, hutazarau.